TANGAZO LA SERIKALI NA 97 la tarehe 17/03/2017

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAGULIO NA MINADA) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI ZA MWAKA, 2017

Jina

Tangazo la Serikali Na 25/2016

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Magulio na Minada) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi za Mwaka, 2017 na zitasomwa pamoja Na Sheria Ndogo za (Ushuru wa Magulio na Minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi za Mwaka, 2016 ambazo zitaitwa Sheria Ndogo Kuu.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Marekebisho ya Kifungu cha 11(3)

3. Kifungu cha 11(3) cha Sheria Ndogo Kuu kinarekebishwa kwa kufuta maneno “isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi laki tatu” yanayosomeka kwenye mstari wa tatu wa kifungu hicho na kuweka maneno mapya yatakayosomeka “isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini (Tsh.50, 000/=)”.

Lakiri ya Halmashauri ya Bariadi ilibandikwa katika Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio la Kikao cha Mkutano wa Baraza la Halmashauri uliofanyika tarehe ………………… mwezi ………………….mwaka 2016 na kubandikwa mbeleya:

ABDALLAH MOHAMED MALELA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi*

RICHARD KIBERITI BUYAMBA,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi*

NAKUBALI

Dodoma,
Tarehe…………….

GEORGE B. SIMBACHAWENE,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tamisemi*